

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KWANZA

30 MACHI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 30 MACHI, 2021

I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:

III. TAARIFA YA SPIKA:



IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA, MB.

Azimio la Bunge la Kuutambua na Kuenzi Mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Utumishi wake uliotukuka.

MHESHIMIWA JOSEPH KIZITO MHAGAMA, MB.

Azimio la Bunge la Kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

V. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

1. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

2. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusiana na ongezeko la vitendo vya ubakaji na udhalilishaji wa Watoto nchini;

- (b) Je, kwa nini Serikali haifanyi tafiti kujua sababu za kesi nyingi kushindwa kuwatia hatiani wabakaji na kuja na mpango mpya wa kudhibiti vitendo hivyo.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

3. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya michezo ya kubahatisha maarufu kama bonanza kulipiwa kodi ya shilingi laki moja tu kwa mwezi na kutolipa *Service Levy* kwa Halmashauri.

WIZARA YA MAJI:

4. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji safi na salama Butiama ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa Baba wa Taifa katika Taifa letu.

**5. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA
KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali italeta Mradi wa Kuhifadhi Mazingira Mufindi katika chanzo cha maji cha Mto Ruaha na Shamba la Miti la Sao Hill.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**6. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Mtwara Pachani – Nallasi – Tunduru itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**7. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI
(UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini daraja la Kisorya – Lugezi litakalounganisha Wilaya za Bunda na Ukerewe litajengwa ili kurahisisha ukuaji wa uchumi wa Wananchi wa Wilaya hizo.

WIZARA YA NISHATI:

8. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Wananchi katika mitaa 30 isiyo na umeme Wilayani Handeni watapatiwa umeme kupitia mradi wa REA.

9. MHESHIMIWA JUMANNE ABDALLAH SAGINI (BUTIAMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itazipatia umeme Kaya na Vitongoji ambavyo havijapatiwa umeme Wilayani Butiama.

WIZARA YA KILIMO:

10. MHESHIMIWA ASSA NELSON MAKANIKA (KIGOMA KASKAZINI):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwekeza yenyewe katika zao la Mchikichi badala ya kuziachia Halmashauri ili kukabiliana na upungufu wa mafuta nchini.

VI. MAAZIMIO YA BUNGE:

Azimio la Bunge la Kuutambua na Kuenzi Mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Utumishi wake uliotukuka; na

Azimio la Bunge la Kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



DODOMA
30 MACHI, 2021

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE